MHE. JAKAYA MRISHO KIKWETE
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

HOTUBA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHESHIMIWA JAKAYA MRISHO KIKWETE, AKIFUNGUA RASMI BUNGE JIPYA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, DODOMA, 30 DESEMBA 2005

Mheshimiwa Spika:

Niruhusu nianze na shukrani. Shukrani zangu za kwanza ni kwa Mwenyezi Mungu aliyetujalia uhai na afya, akatuwezesha kukutana hapa kuzindua rasmi Bunge la Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kutuwezesha kukamilisha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 kwa amani, utulivu na heshima kubwa kwa nchi yetu. Uchaguzi huu umemfanya kila Mtanzania, ndani na nje ya nchi yetu, kutembea kifua mbele.

Kwa mara nyingine nakishukuru sana Chama changu, Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwa heshima kubwa kilichonipa kwa kuniteua niwe mgombea wake wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru wana-CCM wenzangu na wapenzi wa CCM kwa kushiriki kampeni iliyotupa ushindi mkubwa sana. Napenda kuwahakikishia

kuwa sitawaangusha. Utekelezaji wa Ilani yetu ya Uchaguzi upo salama mikononi mwangu.

Kupitia Bunge hili, ninawashukuru wananchi kwa kunipa mimi na Chama changu ushindi mkubwa sana; ushindi uliowatisha wasioielewa Tanzania. Wanaoielewa vizuri Tanzania, Taifa lililoasisiwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume, hawakushangaa sana. Shukrani zangu kwa Watanzania wenzangu wana-CCM na wasio wana-CCM ni ahadi ya kuwatumikia kwa uwezo wangu wote na kutimiza matumaini yao kwangu na kwa Chama chetu, CCM.

Nawashukuru viongozi wa vyama vya upinzani, na vyama vyao, kwa ujasiri wao mkubwa wa kujitokeza kushindana na Chama Cha Mapinduzi na viongozi wake. Uchaguzi sasa umekwisha. Kauli ya wananchi imedhihirika. Tuungane, tuwe kitu kimoja; tujenge na kuendeleza nchi yetu. Mimi naamini kuwa Tanzania yenye amani na uchumi imara, uchumi utakaompa kila raia maisha bora zaidi, ni jambo lenye maslahi kwetu sote na ndiyo azma ya kila mmoja wetu.

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kumkubali mteuliwa wa CCM kwa nafasi ya Spika,

Mheshimiwa Samuel John Sitta, Mb., na pia kwa kukubali uteuzi wangu wa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mb. Naomba mumpe Waziri Mkuu, pamoja na Mawaziri na Naibu Mawaziri nitakaowateua hivi karibuni, ushirikiano mkubwa. Wachangamsheni, lakini watendeeni haki na wapeni ushirikiano.

Mheshimiwa Spika:

Nawapongeza Wabunge wote waliochaguliwa. Ninyi, Waheshimiwa Wabunge, ndio macho na masikio ya wananchi. Mmeaminiwa na kuheshimiwa . Naomba kila siku mnapoingia au kutoka katika Bunge hili, mnapozungumza humu ndani au mnaposikiliza wengine wakizungumza, mnapokuwa macho au mnapofumba macho kutafakari kwa kina, kila mara mkumbuke imani na heshima hiyo kubwa mliyopewa na wananchi.

Nakupongeza sana wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge, na pili kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu. Umepata kazi ya heshima kubwa sana, yenye wajibu mkubwa sana. Unao uwezo na uzoefu wa kuifanya. Hivyo, sina shaka utaimudu vema kazi hiyo, na utaliongoza Bunge hili kwa hekima na busara, ukiwatendea haki Wabunge wote,

na upande wa Serikali pia. Ninakutakia kila la kheri, na ninakuhakikishia ushirikiano kamili katika kazi zako.

Mheshimiwa Spika:

Ninampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar. Sikushangaa, maana amefanya kazi kubwa na nzuri ya kuwatumikia wananchi katika miaka mitano iliyopita. Wananchi wa Zanzibar wanathamini juhudi zake za kulinda heshima na utu wa Wazanzibari wote na kuulinda Muungano wetu. Namhakikishia ushirikiano wangu na wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika:

Navipongeza vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya ya kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa kisiwa cha amani na utulivu wakati wote wa mchakato wa Uchaguzi Mkuu. Wakuu wa vyombo hivyo, makamanda, maafisa, askari, na watendaji wote wameonyesha uaminifu kwa Taifa na uzalendo wa hali ya juu. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika:

Wananchi wengi wameelimika na kufuatilia mchakato wote wa Uchaguzi Mkuu kutokana na kazi kubwa na nzuri iliyofanywa na vyombo vya habari. Vyombo vya habari vimetekeleza vizuri wajibu wao kwa Watanzania, wakati mwingine katika mazingira magumu. Nao nawashukuru na kuwapongeza.

Mheshimiwa Spika:

Serikali ya Awamu ya Nne ambayo nimepewa heshima ya kuiongoza, inaanza kazi wakati nchi ikiwa na hali nzuri kiuchumi, kisiasa na kijamii. Mafanikio hayo yametokana na uongozi imara na thabiti wa Rais Mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.

Napenda kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanyia nchi yetu. Kwangu binafsi, amekuwa mwalimu na mwelekezi ambaye amenijengea uwezo na dhamira ya kuendeleza kazi aliyoianza. Namtakia kiongozi wetu mpendwa, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, afya njema na maisha marefu, yeye, Mama Mkapa, na familia yao. Sitaki kuzungumzia mapumziko yake. Najua dunia itamhitaji sana katika kustaafu kwake na sisi pia vivyo hivyo. Lakini, yeye hasa ni wetu na tuna haki ya kuendelea kumtumia na kuchota kutoka

kwenye kisima chake cha busara, hekima, ujuzi na uzoefu. Matarajio yangu ni kuwa ataturuhusu tufanye hivyo.

Mheshimiwa Spika:

Pongezi zangu za mwisho kwa kutajwa, lakini si kwa umuhimu, ni kwa Tume ya Uchaguzi ya Taifa, na Tume ya Uchaguzi Zanzibar, kwa kazi nzuri sana waliyoifanya katika chaguzi zilizopita. Watazamaji wa uchaguzi wetu, kutoka ndani na nje ya nchi yetu, wote wamekiri kuwa Uchaguzi Mkuu mwaka huu uliendeshwa kitaalamu na kwa ufanisi mkubwa zaidi kuliko miaka iliyopita. Nazipongeza sana Tume zetu hizi. Naomba waendelee kunoa uwezo wao, maana Watanzania-Bara na Zanzibar tunao wajibu wa kihistoria wa kuwa mfano bora barani Afrika na hata kwingineko.

Siasa

Mheshimiwa Spika:

Chama Cha Mapinduzi kimerejeshwa madarakani kwa kura halali za wananchi zilizotupa idhini ya kutawala, tena idhini kubwa isiyo na shaka hata kidogo. Hatutaona aibu kuitumia idhini hiyo, kupitia Bunge hili, kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005.

Ushindi nilioupata mimi, na kwa ujumla ushindi wa CCM, ni kura ya imani kwa CCM, ni kura ya imani kwa sera za CCM, na ni kura ya imani kwa uongozi thabiti, uongozi makini na uongozi usiotetereka wa Rais aliyenitangulia, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na Serikali ya Awamu ya Tatu. Rekodi ya utekelezaji wa Serikali hiyo ndio mtaji wa msingi tulioenda nao kwa wananchi. Rekodi hiyo ilitupa pa kusimama, ikarahisisha kazi yetu ya kukinadi Chama Cha Mapinduzi. Kama mwana-CCM nafurahia sana ushindi wetu. Lakini, nikiwa Rais, napenda niwahakikishie wapinzani kuwa hatuna nia au sera ya kuua vyama vya upinzani. Serikali ya Awamu ya Nne itaendeleza, kwa dhati, mfumo wa siasa wa demokrasia ya vyama vingi. Ushauri wangu kwa wapinzani ni kuwa wasiwe wepesi kutafuta mchawi kila wanaposhindwa uchaguzi. Badala yake nawaomba wajiulize kwa nini Watanzania wamewakataa kiasi hicho. Nina uhakika watapata jibu.

Mheshimiwa Spika:

Ni kweli nchi yetu sasa ni ya demokrasia ya vyama vingi. Lakini ni wazi bado utamaduni wa mfumo huu wa siasa ni mchanga na kwa ujumla haujaimarika vya kutosha. Serikali ya Awamu ya Nne itajitahidi kutimiza wajibu wake katika kujenga na

kuimarisha utamaduni na mfumo wa siasa za vyama vingi. Tutajitahidi kujenga utaratibu na misingi ya mahusiano mema zaidi baina ya vyama vya siasa nchini Tanzania. Tunakihakikishia kila chama uhuru wa kuandaa sera zake na kuzinadi. Hata hivyo, sitegemei kuwa vyama vya siasa vitakuwa na sera za kuligawa, kulihujumu, kulisaliti, kulidhoofisha au kulibomoa Taifa letu.

Hadi sasa tumetegemea zaidi busara za viongozi wa vyama vya siasa. Lakini mimi naamini wakati umefika, kama alivyowahi kusema Rais Mkapa, kuwa tuwe na maadili yatakayotawala shughuli za kisiasa, ambayo hayategemei hiari ya viongozi wa kisiasa waliopo madarakani. Yanakuwa ni maadili na miiko ya lazima, yanayobana kila chama cha siasa, wanachama na viongozi wake, ikiwemo wale wa Chama Tawala.

Tusipofanya hivyo na dalili zimeanza kuonekana wanaweza kujitokeza watu wakavuruga nchi yetu kwa kisingizio cha uhuru wa kisiasa. Serikali ya Awamu ya Nne itaheshimu uhuru huo, lakini bila kuhatarisha amani, utulivu, na utaifa wetu. Hakuna uhuru wa kweli usiokuwa na mipaka. Uhuru bila mipaka ni fujo, na siwezi kukubali nchi mliyonikabidhi kuiongoza itawaliwe na fujo.

Mheshimiwa Spika:

Jambo jingine linalonisumbua linahusu upatikanaji na matumizi ya fedha na michango mingine kwenye uchaguzi. Yameanza kujitokeza mawazo, pamoja na kuanza kujengeka utamaduni, kuwa uongozi unaweza kununuliwa kwa fedha. Kama ni kweli, tusipokuwa waangalifu, nchi yetu inaweza kuwekwa rehani kwa watu wenye fedha za kununua uongozi au wanaoweza kupata fedha za kufanya hivyo. Ni kweli kwamba fedha ni nyenzo mojawapo muhimu katika kufanikisha uchaguzi, kwa kila chama na kwa kila mgombea. Lakini, fedha kutumika kununua ushindi si halali. Kwa maoni yangu hatuna budi kupiga vita utamaduni huu kwa nguvu zetu zote. Ni vema sasa tuanzishe mjadala wa kitaifa na hatimaye kuelewana kuhusu utaratibu halali, ulio wazi, wa chama au mgombea kutafuta fedha za uchaguzi; na utaratibu halali, ulio wazi, wa chama au mgombea kutumia fedha hizo. Na utaratibu tutakaokubaliana uwe ni sehemu ya maadili ya uchaguzi katika uchaguzi wa kiserikali na ndani ya vyama vya siasa.

Majukumu ya Msingi ya Serikali ya Awamu ya Nne

Mheshimiwa Spika:

Tangu tupate Uhuru, kila awamu ya uongozi wa taifa imekuwa na majukumu yake ya msingi.

Awamu ya Kwanza iliyoongozwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, na baadaye akishirikiana na Mzee Abeid Amani Karume, iliunda na kujenga taifa. Wakoloni hawakujenga hisia za utaifa, maana mkakati wao wa kututawala ulikuwa kutudhoofisha kwa kutugawa ili tutawalike kwa urahisi. Mwalimu Nyerere hakurithishwa taifa na wakoloni. Alirithishwa mkusanyiko wa makabila mbalimbali, na watu wa dini na rangi mbalimbali. Mwalimu aliona mbali sana. Akatambua kuwa hata uchumi wa Tanzania ungekua kwa kasi kubwa kiasi gani, iwapo hakuna misingi imara na hisia za dhati za utaifa, baada ya muda tutasambaratika na uchumi huo utakuwa hauna maana.

Mwalimu alirithishwa nchi ya watu maskini, wanaoteseka kwa maradhi, na wasio na elimu ya kutosha kuongoza nchi na kuendesha uchumi wa kisasa. Yeye, na baadaye wakishirikiana na Mzee Karume, wakatoa kipaumbele kwenye vita dhidi ya ujinga, umaskini na maradhi. Mtandao mkubwa wa huduma za jamii, hasa elimu na afya, tunaojivunia leo, una mizizi yake katika falsafa ya maendeleo ya baba wa Taifa. Wengi wetu tutiomo humu ndani, wa makamo yangu, tusingesoma na kufika hapa tulipo kama si kuona mbali na sera nzuri za Baba wa Taifa. Tutamshukuru yeye na Mzee Karume daima.

Awamu ya Pili chini ya Mzee wetu, Ali Hassan Mwinyi, ilifungua milango na kupanua uwanja wa ushiriki wa wananchi kwenye uchumi na siasa. Mzee Mwinyi ni muasisi wa mageuzi ya kiuchumi na kisiasa Tanzania. Alimaliza uhaba wa bidhaa na baadhi ya huduma muhimu uliodhalilisha wananchi. Alipanua sana mipaka ya uhuru wa raia katika maisha yao ya kiuchumi na kisiasa.

Nakumbuka siku moja Mzee Mwinyi alielezea awamu yake kama wakati ambapo mtu anafungua madirisha ya nyumba ili hewa safi iingie ndani. Lakini, akasema, ukifungua madirisha ujue nzi, mbu na wadudu wengine nao wataingia.

Hapo ndipo Awamu ya Tatu ya Rais aliyenitangulia, Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, ilipoanzia. Ilibidi kushughulikia mbu, nzi na wadudu hao. Rais Mkapa alifanya kazi kubwa kurejesha nidhamu kwenye mapato na matumizi ya Serikali. Alipiga vita rushwa kwa zake zote, lakini ndani ya mfumo wa utawala wa sheria. Alirejesha mahusiano mazuri na wahisani wetu na washirika wetu kwenye maendeleo. Aliweka mazingira bora ya uwekezaji, na ukuaji wa uchumi. Aliimarisha msingi wa uchumi mkuu. Bei za kuruka, na fedha za soksi zikaisha. Ameweka misingi imara

ya kuwezesha wananchi kujiendeleza kupitia miradi kama vile TASAF na MKURABITA chini ya mwavuli wa MKUKUTA.

Alikarabati na kupanua sana miundombinu ya elimu, afya, maji na umeme. Na kama sote tujuavyo kazi kubwa ya ujenzi wa barabara na madaraja imefanywa na inaendelea. Kutokana na juhudi za Rais Mkapa, ndani ya nchi na kimataifa, Serikali ya Awamu ya Nne inaanza bila mzigo wa madeni usiobebeka kama alivyoanza yeye. Na, siku ambayo alikuwa ananikabidhi madaraka, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) lilitangaza rasmi kuwa Tanzania ni moja ya nchi ambazo uamuzi wa mwisho umefikiwa wa kutufutia madeni ya nje. Tumshukuru kiasi gani?

Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ilisema kuwa chini ya uongozi wa Rais Mkapa, Tanzania ilifanya vizuri sana kwenye vigezo vyote vya kupewa msamaha huo. Mapema mwaka huu Benki ya Dunia nayo ililinganisha nchi za Kiafrika kwa vigezo vya utawala bora na Tanzania ikaibuka nchi pekee ambayo ilifanya vizuri kwenye vigezo vyote vilivyotumika kupima utawala bora. Nauliza tena. Watanzania tumshukuru kiasi gani Rais Mkapa?

Mheshimiwa Spika:

Baada ya shukrani hizo, sasa ni wakati wa kubainisha majukumu ya msingi ya Serikali ya CCM ya Awamu ya Nne.

Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 imetamka bayana majukumu mawili ya msingi.

- Kwanza, kuitoa Tanzania kutoka kwenye dimbwi la uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuiingiza katika mkondo wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea.

- Pili, kuwashirikisha wananchi wote kwa njia ya uwezeshaji katika ujenzi wa uchumi na kuutokomeza umaskini.

Mheshimiwa Spika:

Kwa kuzingatia majukumu haya ya msingi, na mbinu na mikakati mbalimbali ya kuyatekeleza, Watanzania watarajie mambo kumi yafuatayo katika miaka mitano ijayo:

1. Serikali ya Awamu ya Nne itahakikisha kuwa Amani, Utulivu na Umoja wa nchi yetu na watu wake vinadumishwa;

2. Serikali ya Awamu ya Nne itadumisha na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana tangu Serikali ya Awamu ya Kwanza hadi leo;

3. Serikali ya Awamu ya Nne itaendeleza vita dhidi ya umaskini, ujinga na maradhi, tena kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya;

4. Serikali ya Awamu ya Nne itatimiza ipasavyo wajibu wake wa utawala na maendeleo, na itaendesha dola kwa misingi ya utawala bora na uwajibikaji; utawala wa sheria unaoheshimu na kulinda haki za binadamu;

5. Serikali ya Awamu ya Nne itaimarisha uwezo wake wa kulinda maisha na mali za raia wake. Tutapambana na uhalifu wa kila aina, na majambazi hayataachwa yatambe yatakavyo;

6. Serikali ya Awamu ya Nne itahakikisha mipaka ya nchi yetu ipo salama. Hatutamruhusu mtu au nchi yeyote kuchezea mipaka ya nchi yetu na uhuru wetu;

7. Serikali ya Awamu ya Nne itafanya kila iwezalo kuhakikisha Tanzania ina mahusiano

mazuri na mataifa yote duniani, pamoja na mashirika ya kimataifa na kikanda;

8. Serikali ya Awamu ya Nne itajali sana maslahi na mahitaji ya makundi maalum katika jamii kama vile wanawake, vijana, watoto, wazee, walemavu na yatima;

9. Serikali ya Awamu ya Nne itaongoza mapambano mapya ya kuhifadhi mazingira ili vizazi vijavyo virithi nchi nzuri, na msingi imara wa maendeleo endelevu; na

10. Serikali ya Awamu ya Nne itaendeleza michezo, na shughuli za utamaduni na burudani.

Umoja wa Kitaifa

Mheshimiwa Spika:

Umoja wa kitaifa ni mhimili mkuu wa amani na utulivu. Na Watanzania wanaenzi sana umoja wao, utulivu wao na amani yao. Naamini ndio maana wameacha kuvipigia kura vyama vinavyohusishwa na vurugu, na/au vyama ambavyo msimamo wao kuhusu Umoja na Muungano unatiliwa mashaka.

Umoja wa kitaifa wa Tanzania una pande mbili. Upande wa kwanza ni Muungano wetu; umoja wa nchi zetu mbili huru zilizoungana kuunda Jamhuri ya Muungano. Muungano wetu sasa una zaidi ya miaka 41, ni wa pekee barani Afrika. Pamoja na kuwepo matatizo ya hapa na pale Muungano bado ni imara na ni wa kujivunia. Upande wa pili wa umoja wa kitaifa ni umoja wa raia wenyewe, wanaojihisi wote ni Watanzania kwanza, bila kujali tofauti zao za kabila, dini, rangi, jinsia au eneo atokalo mtu.

Kazi mojawapo ya msingi ya Serikali nitakayoiunda ni kulinda, kudumisha, kuendeleza na kuimarisha Muungano wetu, kwa kufanya yafuatayo:

1. Kwa jumla tutakuwa makini na wepesi katika kushughulikia matatizo ya Muungano. Tutayazungumza kwa uwazi na kuchukua hatua muafaka kwa wakati muafaka;

2. Nitampunguzia Makamu wa Rais majukumu ya kuondoa umaskini ili apate muda wa kutosha wa kushughulikia masuala ya Muungano;

3. Nitaimarisha taratibu zilizoanzishwa na Serikali zilizopita za kujadili, kuainisha na kutatua matatizo ya Muungano; na

4. Nitaangalia upya mchango wa Serikali ya Muungano katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Zanzibar, bila kuathiri haki na mamlaka kamili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mambo ambayo si ya Muungano.

Mheshimiwa Spika:

Kwa upande mwingine, umoja wa Watanzania unahusu umoja miongoni mwa wananchi, watokanao na makabila zaidi ya 120, na wa maeneo, rangi na dini mbalimbali. Lakini Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere aliwafanya Taifa moja, lenye umoja wa kitaifa unaopigiwa mfano kote barani Afrika na duniani. Hili ni jambo jema, jambo la kujivunia na jambo la kudumishwa na kuendelezwa kwa nguvu na bidii zetu zote.

Ipo hofu ya kweli miongoni mwa Watanzania kuwa bado wapo miongoni mwetu watu wanaotaka kuturudisha tulikotoka, tuanze tena kuulizana na kubaguana kwa misingi ya kabila zetu, rangi zetu, dini zetu, na maeneo tunayotoka.

Nawasihi sana wanaowania uongozi, kuanzia ngazi ya chini kabisa hadi ngazi ya kitaifa uwe uongozi wa kiserikali, uongozi wa kisiasa au uongozi wa kidini wasitumie ubaguzi wa aina yeyote ile. Hawatavumiliwa na hawataachwa waigawe nchi.

Mheshimiwa Spika:

Nachukua uongozi wa Taifa letu nikiwa nasononeshwa sana na mpasuko wa kisiasa kati ya Unguja na Pemba, na pengine kati ya Pemba na sehemu nyingine za jamhuri yetu. Matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa 2005 yametukumbusha tena mpasuko huo ambao naamini chanzo chake ni cha kihistoria. Lakini historia hiyo ni ya wanadamu, na wanadamu hawalazimiki kuwa wafungwa wa historia yao. Iweje Wapemba hawa ambao ni hodari wa kutumia fursa ya Muungano wetu kwa kuishi na kufanya biashara na kuwekeza katika pembe zote za jamhuri yetu wawe hao hao wanaojitenga kisiasa kwa kiwango tulichoshuhudia kwenye Uchaguzi Mkuu?

Wakati umefika sasa wa kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa mpasuko huo. Nategemea ushirikiano mzuri kutoka kwa wanasiasa wa Tanzania-Zanzibar. Natambua kuwa uamuzi wa mwisho kuhusu hatma ya siasa na utawala Zanzibar ni wa Wazanzibari

wenyewe. Lakini, Jamhuri yetu ni moja, na yanayotokea Zanzibar yanatugusa sote. Pengine leo ni zaidi kuliko ilivyokuwa katika historia wakati ulipokuwepo msemo kuwa zumari likipigwa Zanzibar wanacheza mpaka bara. Hivyo, basi, nitakuwa tayari kuanzisha, kuwezesha na kusaidia mjadala mpana juu ya mustakabali wa kisiasa Zanzibar. Naamini kuwa kuendeleza pale utekelezaji wa Muafaka ulipoishia kabla ya uchaguzi kutasaidia sana. Hata hivyo, kama hapana budi, tutatafuta mikakati na mbinu nyingine mpya. Najua si kazi rahisi, lakini nchi hii ni yetu sote. Nakusudia kufanya kila lililo ndani ya uwezo wangu ili siku awamu yangu ya uongozi wa jamhuri yetu ikifika ukingoni nisiiache hali hii ya mpasuko wa kisiasa kama nilivyoikuta.

Mheshimiwa Spika,
Waheshimiwa Wabunge:

Serikali ya Awamu ya Nne inakusudia, miongoni mwa mambo mengine, kuimarisha utaifa wetu kwa kufanya mambo kumi yafuatayo:

1. Kutumia mfumo wa elimu kujenga na kuimarisha umoja wa kitaifa, ikiwemo, kutenga Shule za Sekondari za Kitaifa zitakazochanganya

kwa makusudi wanafunzi wenye vipaji mbalimbali kutoka pembe zote za Tanzania;

2. Kuandaa mitaala ya somo la uraia itakayopanda mbegu za uzalendo na umoja wa kitaifa katika ngazi zote za elimu;

3. Kuzipa changamoto shule za mashirika ya dini, isipokuwa seminari, kupokea wanafunzi wa dini zote;

4. Kuendeleza kazi nzuri iliyoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tatu ya kufufua Jeshi la Kujenga Taifa;

5. Kujenga muafaka baina ya vyama na makundi ya jamii juu ya utambuzi wa, na kuheshimu, tunu za kitaifa kama vile haki, usawa, umoja na mshikamano;

6. Kutumia michezo, nyimbo na sanaa kuimarisha hisia za utaifa na kujenga uzalendo na kuipenda nchi;

7. Kueneza na kuruhusu matumizi ya alama za kitaifa kama mambo ya kila raia kujivuna nayo na kuyaheshimu sana;

8. Kujenga na kuimarisha mahusiano kati ya dini, vyama vya siasa na makundi mbalimbali ya jamii;

9. Kuteua Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais atakayeshughulikia mahusiano kati ya vyama vya siasa, dini na makundi mbalimbali ya jamii; na

10. Kuimarisha utaratibu wa mazungumzo ili kutatua mapema migogoro katika jamii.

Amani na Utulivu

Mheshimiwa Spika:

Zipo sababu kwa nini nchi yetu imekuwa, kwa kiwango kikubwa, kisiwa cha amani na utulivu katika bahari iliyotibuka. Mojawapo ya sababu hizo, kama nilivyosema, ni sera ambazo kwa makusudi zilijenga hisia za umoja, na hazikuwabagua wala kuwanyima haki Watanzania kwa sababu za dini, rangi, kabila, jinsia au eneo wanakotoka. Nitawatarajia watakaokuwa kwenye Serikali nitakayoiunda wasiwabague wananchi kwa sababu yoyote ile, na wawe watetezi thabiti wa haki za binadamu.

Ningependa tufike mahali tuwe na maadili na miiko ambapo kiongozi wa chama chochote, kiwe Chama Tawala au cha upinzani; chama cha hiari au chama cha wafanyakazi; chama cha kitaaluma au chama kingine chochote kile, atajiuzulu mara moja ikithibitika kuwa anajihusisha na sera za ubinafsi, ubaguzi, uchochezi, chuki na zote zinazobomoa umoja wa kitaifa, au kuhatarisha amani na utulivu wa nchi yetu.

Utawala Bora

Mheshimiwa Spika:

Serikali nitakayoiongoza itazingatia na kuendeshwa kwa misingi ya utawala bora, uwazi na uwajibikaji. Tutaheshimu utawala wa sheria, na kati ya mihimili mikuu ya dola, yaani Utawala, Bunge na Mahakama. Tutaheshimu uhuru wa Mahakama na Bunge; tutatimiza ipasavyo wajibu wetu; na tutawezesha mihimili hiyo kufanya kazi zake ipasavyo. Serikali ya Awamu ya Nne itaimarisha utendaji Serikalini na kupambana na maovu katika jamii bila woga wala kuoneana muhali.

Rushwa

Tutaongeza kasi ya kupambana na rushwa kisayansi kwa kushambulia kiini chake, na kuziba

mianya yake. Kwa kadri mapato ya Serikali yanavyoongezeka ndivyo tutakavyoongeza mishahara na kuboresha maslahi ya watumishi wa umma ili kupunguza vishawishi vya rushwa. Tutaendelea pia kuongeza uwazi katika maamuzi ya Serikali. Tutaimarisha uwezo wa kifedha na kiutendaji wa taasisi zilizo mstari wa mbele kwenye vita dhidi ya rushwa, hususan Taasisi ya Kuzuia Rushwa, jeshi la Polisi na Mahakama. Lakini yote hayo ni bure iwapo wananchi hawatajitokeza kusaidia vyombo hivyo. Naomba ushirikiano huo kutoka kwa wananchi.

Katika harakati za kupambana na rushwa yapo mambo mawili mengine ambayo tutayaangalia kwa karibu. La kwanza ni mikataba. Tutaangalia upya taratibu za mikataba mbalimbali inayoiingiwa na Serikali, mashirika ya umma na idara zinazojitegemea kwa nia ya kuongeza uwazi na uwajibikaji. Mikataba ni mwanya mkubwa wa rushwa, hasa zile kubwa kubwa. Nadhani wakati umefika wa kuwa na taratibu thabiti za kubana na kuziba mwanya huu.

Kadhalika, hatuna budi kuchukua hatua thabiti za kuzuia watumishi wa umma kutumia nafasi zao kujitajirisha na kujilimbikizia mali. Sisemi kwamba ni haramu mtu kuwa tajiri au kuwa na mali. Ni jambo

jema kwani sera yetu inalenga kuinua hali ya maisha ya watu kwa kupambana na umaskini wa kipato. Ninachosema mimi kuwa ni haramu ni kutumia nafasi yako ya utumishi au uongozi wa umma kujipatia manufaa ya kujitajirisha au kujilimbikizia mali.

Jambo hili ndilo linalokera sana watu kuona mtu ambaye hana chochote lakini miezi michache tu baada ya kuwa Mbunge au Waziri, Katibu Mkuu au Mkurugenzi, au Mkuu wa Idara, ana majumba ya fahari, madaladala, teksi bubu, anaishi maisha ya kifahari, na kadhalika. Wananchi wanayo haki kuhoji, na wanayo haki kupata majibu. Kwa vyo vyote, inatia shaka ya kuwepo mazingira ya rushwa. Serikali ya Awamu ya Nne haina budi ichukie tabia hiyo na kila mmoja wetu awe askari wa kupambana nayo. Maombi yangu kwa Tume ya Maadili ya Viongozi ni kuwa wasione haya kutuuliza jinsi tulivyozipata mali tunazosema tunazo. Tusingoje mpaka mtu aje kulalamika. Nitawasaidia kujenga uwezo wa kufanya hivyo.

Utendaji Serikalini

Mheshimiwa Spika:

Dhana ya utawala bora ni pana sana; ni zaidi ya vita dhidi ya rushwa. Serikali ya Awamu ya Nne

itashughulikia maeneo yote ya utawala bora. Tutahimiza utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa ustadi, kwa haraka na kwa ufanisi. Tunataka watendaji wa Serikali wenye uadilifu wa hali ya juu na wenye kuzingatia misingi ya uwajibikaji na maadili bora ya kazi; watendaji wenye ari, moyo, na msimamo wa dhati kuhusu utumishi wa umma na huduma bora kwa umma.

Nitataka watakaokuwa kwenye Serikali ya Awamu ya Nne wajijengee tabia ya mara kwa mara wao wenyewe kujiuliza iwapo kwa maamuzi yao, kwa vitendo vyao na kwa tabia zao wanajenga au wanabomoa heshima ya Serikali machoni pa wananchi.

Natambua tatizo na malalamiko ya watumishi wa ummna kuhusu mishahara na maslahi yao. Tutaliangalia. Tutalishughulikia. Nakusudia mapema iwezekanavyo niteue Tume ya Kuboresha Maslahi ya Watumishi wa Umma, lengo likiwa ni kuwa na mkakati wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu wa kuongeza mishahara na kuboresha maslahi yao. Hatua hizo zitawawezesha wafanyakazi wa umma kumudu maisha yao na kupunguza manung'uniko na milipuko ya migogoro.

Mahakama

Mheshimiwa Spika:

Ili kuimarisha utoaji haki, jitihada kubwa zimefanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu kuimarisha Mahakama na kuanzisha vitengo maalum vya Mahakama Kuu hususan, Mahakama ya Ardhi na Mahakama ya Biashara. Serikali nitakayoiunda, pamoja na kuheshimu uhuru wa Mahakama itatimiza ipasavyo wajibu wake na kuimarisha miundombinu ya kutoa haki kwa kuongeza idadi ya watumishi, kuwaendeleza kitaaluma, kukarabati majengo yaliyopo na kujenga mapya, na kupeleka huduma za utoaji haki karibu zaidi na wananchi.

Mapato na Matumizi ya Serikali

Mheshimiwa Spika:

Kusimamia vizuri mapato na matumizi ya Serikali nayo ni sehemu ya utawala bora. Isitoshe, utekelezaji mzuri wa jukumu hilo ndio unaipa Serikali uwezo wa kutekeleza mengine yote inayopaswa au inayokusudia kuyatekeleza. Serikali ya Awamu ya Tatu, chini ya uongozi shupavu wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, iliongeza mapato ya Serikali mara tano sambamba na kuweka mfumo mpya na wa kisasa wa kudhibiti matumizi, na kuongeza uwazi katika bajeti ya Serikali.

Napenda kuwaahidi Watanzania kuwa Serikali ya Awamu ya Nne itashika uzi huo huo. Hatutalegeza kamba hata kidogo. Hatutavumilia wanaokwepa kulipa kodi stahiki za Serikali au wabadhirifu wa fedha na mali za umma.

Mheshimiwa Spika:

Nidhamu katika matumizi nayo ni sehemu ya uwajibikaji na utawala bora, na inachangia kudhibiti mfumuko wa bei. Sheria ya Fedha, na Sheria ya Manunuzi ya Umma, lazima zifuatwe. Watakaokiuka wachukuliwe hatua za nidhamu. Wasiorejesha masurufu ya safari nao wasivumiliwe.

Kazi za Serikali kwenye Uchumi wa Soko

Mheshimiwa Spika:

Utawala bora ni pamoja na Serikali kufanya vizuri kazi zake nyingine muhimu katika mazingira ya uchumi wa soko. Jukumu la msingi la Serikali ni kutengeneza mazingira mazuri kwa uchumi kukua na biashara kustawi. Kwa sababu hiyo, Serikali ya Awamu ya Nne itatekeleza mambo manane yafuatayo:

1. Kuweka sera na mazingira bora ya kuvutia uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi;

2. Kuweka sera nzuri zinazowezesha ukuaji wa uchumi wa kisasa;

3. Kuweka mfumo mzuri wa usimamizi wa mazingira ili kulinda uhai wa binadamu na viumbe hai;

4. Kuweka mifumo bora ya kusuluhisha haraka tofauti na migogoro kati ya wawekezaji au wafanyabiashara, au tofauti za kibiashara baina ya mtu na mtu au kampuni na kampuni;

5. Kuweka utawala mzuri wa sheria na wa haki;

6. Kuwa na taasisi za kudhibiti na kusimamia viwango vya huduma na bidhaa;

7. Kuwa na sera nzuri za kifedha ili kuhamasisha uwekezaji na uzalishaji; na

8. Kutekeleza kwa dhati sera ya uwezeshaji wa wazawa ili na wao washiriki kwa ukamihfu katika kumiliki na kunufaika na raslimali na fursa za nchi yao.

Uchumi Endelevu wa Kisasa Unaokua

Mheshimiwa Spika:

Kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kazi ya msingi ya Serikali ya Awamu ya Nne ni

kukuza uchumi kwa lengo la kuongeza kipato cha Watanzania ili waishi maisha bora zaidi.

Serikali ninayoingoza itatoa kipaumbele katika kujenga uchumi endelevu, wa kisasa, unaokua. Serikali ya Awamu ya Tatu imefanya kazi kubwa katika eneo hilo, na kutuachia msingi imara ambao sisi tutajenga juu yake. Hatutabomoa msingi huo bali Serikali itatumia mafanikio hayo kama nyenzo ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika:

Sekta binafsi ndiyo mhimili wa uchumi wa nchi yetu hivi sasa. Serikali ya Awamu ya Tatu imeweka mazingira mazuri ya ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi wa Taifa. Aidha, Serikali ya Awamu ya Tatu imejenga mahusiano mazuri na sekta binafsi ambayo sasa imepewa fursa ya kushirikiana na Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini. Serikali ya Awamu ya Nne itaendeleza kazi hiyo nzuri. Tutajitahidi kuwa karibu na sekta binafsi kwa maslahi ya nchi yetu.

Kilimo

Mheshimiwa Spika:

Kwa muda mrefu ujao, kilimo kitaendelea kuwa mhimili wa uchumi wetu. Sekta hii ndiyo

inayoajiri watu wengi na ndiyo inayotuhakikishia upatikanaji wa chakula, bidhaa za kuuza nje na malighafi za viwanda. Vilevile, uhai na maendeleo ya sehemu kubwa ya wananchi yanategemea kilimo. Hivi sasa, Serikali inatoa ruzuku kwenye mbolea na vilevile unafuu wa kodi kwenye pembejeo za kilimo na mifugo. Mpango huo utaendelezwa na kuimarishwa zaidi.

Aidha, Serikali itahakikisha kuwa Mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji unaongezewa fedha na wataalam ili tupanue maeneo yanayotumika hivi sasa kwa kilimo cha umwagiliaji maji. Vilevile, tutahakikisha kuwa utaalam wa asili wa kilimo cha umwagiliaji unafufuliwa, pamoja na miundombinu yake. Huduma muhimu za ugani na masoko zitapewa kipaumbele na msukumo maalumu.

Mheshimiwa Spika:

Tutachukua hatua za dhati kuboresha ufugaji wetu. Hatuna budi tutoke kwenye uchungaji wa kuhama-hama na kuwa wafugaji wa kisasa. Tutachukua hatua za kuboresha malisho na huduma za madawa, majosho na minada.

Ni wajibu wa Mamlaka zote za mikoa na wilaya nchini, hususan kule kwenye mifugo mingi,

kutenga maeneo maalum kwa ajili ya mifugo katika mipango yao ya matumizi ya ardhi. Tanzania ina mifugo mingi sana, na tukiboresha ufugaji, itatoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa na maendeleo ya wafugaji. Uvuvi nao ni eneo ambalo hatujatumia ipasavyo rasilimali zilizopo kwa maendeleo yetu. Hivyo, Serikali itawawezesha wavuvi wengi iwezekanavyo kupata zana bora na vifaa muhimu vya uvuvi wa kisasa ili waweze kutumia kwa ukamilifu eneo la bahari, maziwa na mito ambalo tumejaliwa kuwa nayo.

Viwanda Vidogo na vya Kati

Mheshimiwa Spika:

Uchumi wa nchi yoyote iliyoendelea ulianza na kilimo na kisha kuwa wa viwanda. Nasi hatuna budi kuelekeza nguvu na kuweka mkakati maalum katika kukuza na kuendeleza viwanda nchini.

Viwanda-vikubwa, vidogo na vya kati-vina uwezo mkubwa wa kutoa nafasi za ajira, lakini vilevile vinasaidia kusindika mazao ya kilimo, kuyaongezea thamani na kuzuia yasiharibike wakati wa mavuno. Serikali ya Awamu ya Nne itatengeneza mkakati kabambe wa kutekeleza sera ya viwanda nchini. Wakati huo huo, Serikali itajitahidi kuwawezesha wazalishaji wadogo na wa kati

kuongeza mitaji yao, kuingiza nchini teknolojia bora zaidi na kuwawezesha kufikisha bidhaa zao kwenye masoko.

Serikali itaendeleza na kuimarisha utoaji wa mikopo kwa viwanda vidogo na vya kati chini ya mpango wa mikopo kwa sekta hiyo ambao unasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania na ambao umeanzishwa katika Mwaka wa Fedha 2004/2005. Shirika la Viwanda Vidogo litapewa uwezo zaidi wa kumudu kazi za kutoa elimu, ushauri, uwezeshaji na usimamizi.

Sayansi na Teknolojia

Mheshimiwa Spika:

Uchumi wa kisasa ni ule unaoendeshwa kwa kutumia maarifa ya kisasa, yaani kwa sayansi na teknolojia. Serikali ya Awamu ya Nne itahimiza matumizi ya sayansi na teknolojia, na kuwekeza katika utafiti. Aidha, Serikali itashirikiana na sekta binafsi kuhakikisha kuwa fedha zinapatikana kwa ajili ya taasisi na asasi mbalimbali zinazoshughulikia utafiti wa kiteknolojia. Mfuko wa Taifa wa Sayansi na Teknolojia utaimarishwa kwa kuongeza mchango wa Serikali na kuwahamasisha wadau wengine kuchangia.

Mheshimiwa Spika:

Teknolojia ya habari na mawasiliano nayo ni mhimili muhimu wa ujenzi wa uchumi na kisasa. Aidha, teknolojia hii imewezesha elimu, taarifa na habari kuvuka mipaka na hivyo kusaidia kupunguza pengo la habari na elimu lililopo kati ya nchi zilizoendelea na zile zinazoendelea. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, tutaongeza kasi ya kuandaa mazingira yatakayotuwezesha kutumia teknolojia hii.

Uchumi Unaoshirikisha Raia Wengi

Mheshimiwa Spika:

Tanzania ni nchi maskini na watu wake wengi wanaishi katika maisha magumu. Wapo Watanzania wachache waliofanikiwa, na tayari dalili za tofauti za kitabaka zimeanza kujitokeza katika jamii ya nchi yetu. Tofauti hizo zisiposhughulikiwa zinaweza kuwa chanzo cha migogoro na mitafaruku katika jamii.

Jawabu si kuwanyang'anya walio nacho na kuwagawia wasio nacho. Tutakuwa tunagawana umaskini, na hivyo hakuna atakayekuwa amefanikiwa. Jawabu sahihi ni kuwasaidia wasio nacho wajikwamue, na wainue hali za maisha yao. Changamoto kubwa ni jinsi gani tunaongeza fursa kwa wasio nacho, na kuchochea utayari wao kutumia fursa hizo.

Mheshimiwa Spika:

Kurekebisha na kutengemaza uchumi ni hatua ya mwanzo tu katika safari ndefu ya kukuza uchumi na kupunguza maskini. Serikali ya Awamu ya Nne itaendelea na hatua inayofuata ya kuongeza ushiriki wa Watanzania walio wengi katika uchumi wa Taifa lao. Wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwanza juhudi zilikuwa kuwafanya wananchi wamiliki uchumi wa Taifa lao kupitia mashirika ya umma. Leo tunataka kufikia lengo hilo hilo la wananchi kumiliki sehemu kubwa ya uchumi wa Taifa lao, moja kwa moja, au kupitia vyama huru vya ushirika.

Mheshimiwa Spika:

Serikali ya Awamu ya Nne itashughulikia vizingiti mbalimbali vinavyowazuia Watanzania walio wengi kushiriki. Aidha, tutaendelea kuboresha mazingira ya biashara ili kuziwezesha biashara ndogo na za kati zikue, zitoe nafasi za ajira na kuongeza ushiriki katika uchumi wa kisasa. Kwa kifupi Serikali ya Awamu ya Nne itaboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa ajili ya wafanyabiashara na wawekezaji wadogo wadogo, kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

1. Kuandaa utaratibu mzuri zaidi wa kutoa leseni za biashara;

2. Kurekebisha mifumo ya mamlaka za udhibiti ili mamlaka hizo ziendelee kukidhi matakwa ya udhibiti wenye manufaa na wakati huo huo mamlaka hizo zitoe nafasi kwa sekta binafsi kukua;

3. Kuandaa mazingira mazuri ya kufikisha taarifa muhimu kuhusu masoko, kuhusu ubora wa viwango vinavyotakiwa, na kuhusu masharti mengineyo kwa wafanyabiashara na hasa wafanyabiashara wadogo na wa kati;

4. Kuitaka mikoa ianzishe vituo vya kufanikisha biashara na uwekezaji mikoani, pamoja na Mabaraza ya Biashara ya Mikoa;

5. Kuboresha mazingira ya biashara na ujasiriamali, ikiwemo kutoa msaada na upendeleo maalum kwa mikopo midogo midogo na ya kati hasa kwa vijana, wanawake na Watanzania wanaohangaika kujikwamua kimaisha;

6. Kuboresha miundombinu inayogusa shughuli za wafanyabiashara wadogo na wa kati;

7. Kuhamasisha, kuhimiza na kutoa motisha kwa shughuli za usindikaji nchini ili kuongeza thamani ya mauzo nje; na

8. Kuhamasisha, kuhimiza na kutoa motisha kwa mafunzo ya kiufundi yanayolenga kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji ikiwemo uzalishaji wa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika:

Tutawezesha Watanzania kwa makundi. Kundi la kwanza ni la Watanzania wasomi, walio ndani au nje ya nchi yetu. Zamani ilikuwa mtu ukitoka Chuo Kikuu, kazi ya Serikali inakungoja. Leo hali si hiyo. Serikali inaweza kukusomesha, lakini haikupi ahadi ya kazi. Wengi inabidi watafute kazi kwenye sekta binafsi, au wajiajiri wenyewe. Na wapo ambao wanahangaika na kusaga lami japo wamesoma vizuri na kuwa na ujuzi wenye soko. Kwa mfano utamkuta mtu anayo shahada ya kilimo, ufugaji au uvuvi lakini yuko mjini anatafuta kazi ya kuajiriwa, na kukaa ofisini kwenye kiyoyozi.

Napenda leo nitoe changamoto na ahadi kwa wasomi wetu hao, wenye fani mbalimbali kama vile kilimo, mifugo, uvuvi, uhandisi, ubunifu wa majengo, sheria, uhasibu na kadhalika. Katika dunia

ya utandawazi na ushindani unaoambatana nao, Watanzania wasomi watabaki nje iwapo hawatakuwa wabunifu zaidi, wakaungana na kuanzisha kampuni kubwa za wazalendo. Bila hivyo hawataweza kuhimili ushindani wa makampuni yaliyokwisha kuimarika au yanayotoka nje ya nchi.

Lakini wakikubali kuungana, na kuanzisha kampuni kubwa zinazoendeshwa kwa misingi halisi ya kibiashara, na sio ubabaishaji, Serikali, kupitia vyama vya taaluma zao, itawaunga mkono, itawasaidia na itawawezesha. Serikali ya Awamu ya Nne itakaribisha mawazo kutoka kwa vyama vya kitaaluma juu ya namna bora ya Serikali kufikia lengo hilo. Ninataka wasomi wetu waweze kuhimili ushindani na wawe kiini cha wajasiriamali wasomi na wakubwa nchini.

Kundi la pili la Watanzania tutakaowasaidia na kuwawezesha ni la wenye miradi midogo sana, miradi midogo na miradi ya ukubwa wa kati. Mazuri mengi yamefanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu, kama vile sera ya uwezeshaji wananchi, sera ya uwekezaji mdogo na wa kati, na mfuko wa udhamini kwa mikopo ya mitaji midogo na ya kati. Yote haya, na mengine mengi, tutayaendeleza kwa jitihada kubwa.

Kundi la tatu ni la wakulima wadogo, wavuvi wadogo na wafugaji wadogo. Hatuwezi kushinda umaskini bila kuwasaidia watu wa kundi hili ambao ndio wengi zaidi. Lazima tuchukue hatua za makusudi za kuwawezesha wajikwamue na hali ya umaskini na uduni wa maisha. Nitahitaji kuona ubunifu wa hali ya juu kutoka kwa nitakaowakabidhi kusimamia sekta hizi kufanikisha azma yetu hii.

Mheshimiwa Spika:

Yote haya yatawezekana tu iwapo Watanzania watabadili mtazamo wao kuhusu nafasi yao, na nafasi ya Serikali, katika kukuza uchumi wa Taifa na uchumi binafsi. Lazima sasa Watanzania wawe wajasiriamali na watumie vizuri fursa za uwezeshaji na uwekezaji zinazowekwa na Serikali. Waswahili husema, ukibebwa na wewe shikilia. Maisha bora hayaletwi na Serikali peke yake; yanaletwa kwa ubia kati ya Serikali na wananchi. Naomba tuimarishe ubia huo katika Awamu ya Nne ya Uongozi wa Taifa letu.

Ajira na Viwanda

Mheshimiwa Spika:

Wakati wa kampeni tulijiwekea lengo la kuongeza nafasi za ajira milioni moja katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Nafasi hizi za ajira zinatarajiwa kutoka Serikalini na katika sekta binafsi.

Upanuzi wa sekta za afya, elimu, kilimo, ujenzi wa nyumba na barabara, usindikaji wa mazao na bidhaa asilia, samaki, na utalii ndilo tumaini kuu la ajira. Aidha, matarajio mengine makubwa ya ajira ni kutoka katika sekta isiyo rasmi, yaani ajira binafsi. Tunasisitiza ahadi yetu ya kuchukua hatua thabiti za kuwasaidia vijana, wanawake na Watanzania kupata mikopo na mitaji ya kuwawezesha kujiajiri. Lengo letu ni kuwa kila raia awe na chanzo cha uhakika cha kipato, na kuibua maeneo mapya ya kuwapatia ajira wananchi wengi zaidi.

Serikali ya Awamu ya Nne itaendeleza pia juhudi za kuhimiza, na kuwezesha, uanzishwaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa kama vile vya nguo na vya kuunganisha bidhaa za matumizi ya nyumbani vyenye uwezo mkubwa wa kutoa nafasi za ajira. Serikali ya Awamu ya Tatu ilibuni mradi uitwao Tanzania Mini-Tiger Plan 2020 ambao kwa kutumia maeneo maalum ya uchumi utaongeza mauzo nje ya nchi, na kuongeza haraka nafasi za ajira. Serikali ya Awamu ya Nne itautekeleza mradi huo kwa ukamilifu.

Ushirika

Mheshimiwa Spika:

Ushirika ni nguzo muhimu ya kuwawezesha wanyonge kuwa na sauti na hivyo kuweza

kupambana na umaskini. Serikali ya Awamu ya Tatu imefanya kazi kubwa na nzuri ya kuunda upya ushirika nchini kwa kuhuisha sera na sheria ili kuweka mazingira yatakayochochea kujengeka kwa vyama huru vya ushirika vinavyonilikiwa na kuendeshwa na wanaushirika wenyewe. Serikali ninayoiongoza itaendeleza juhudi hizo pamoja na kuendelea kuwahamasisha na kuwaelimisha wananchi kujiunga na vyama hivyo.

Huduma ya jamii
Elimu

Mheshimiwa Spika:

Hakuna taifa lililopata maendeleo bila kuendeleza elimu. Hivyo, kuendeleza elimu nchini itakuwa agenda muhimu ya Serikali ya Awamu ya Nne. Kazi kubwa ya kupanua miundombinu ya elimu nchini imefanyika katika miaka kumi iliyopita chini ya Serikali ya Awamu ya Tatu. Uandikishaji wa wanafunzi, wa kike nawa kiume, katika ngazi zote za elimu umeongezeka sana. Serikali ya Awamu ya Nne itachukua hatua zitakazowezesha malengo kumi na moja yafuatayo kufikiwa:-

1. Kuendelea kuandikisha watoto wote wa rika lengwa la kuanza shule;

2. Kuboresha taaluma ili kuongeza viwango vya kufaulu kwa ngazi zote;

3. Kuongeza ajira ya walimu wa elimu ya msingi na sekondari ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi;

4. Kushirikiana na wazazi na wadau wengine wa elimu kujenga majengo muhimu ya vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, maabara na vyoo;

5. Kuongeza ruzuku inayotolewa hivi sasa kwa ajili gharama za kuendesha shule;

6. Kuimarisha taasisi za kudhibiti ubora wa elimu inayotolewa;

7. Kutoa fursa na motisha kwa sekta binafsi, taasisi za dini na mashirika binafsi yanayowekeza katika elimu;

8. Kuimarisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu ili iweze kutoa mikopo kwa wahitaji wengi zaidi;

9. Kujenga angalau chuo kikuu kingine kipya; na

10. Kuhakikisha kuwa mafunzo ya ufundi stadi yanaendelezwa na kuimarishwa kama mkakati wa kupambana na tatizo la ajira.

11. Kuboresha maslahi ya walimu katika shule na vyuo hapa nchini.

Maji

Mheshimiwa Spika:

Tatizo la maji ndicho kilio kikubwa cha Watanzania mijini na vijijini. Ndiyo kero nambari wani. Serikali za awamu zote zimefanya jitihada kubwa kukabiliana na tatizo hilo. Serikali ya Awamu ya Nne inakusudia kulikabili tatizo hili kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Serikali itaweka msukumo mpya katika kuwawezesha wananchi wengi zaidi mijini na vijijini kupata maji safi na salama.

Ni makusudio yangu kuwa tuwe na Mpango Kabambe wa Maji kwa nchi nzima. Mpango ambao utajumuisha mikakati na mbinu mpya za kutekeleza kwa kasi Sera ya Maji na kutatua tatizo la maji. Aidha, Serikali itachukua hatua za kuziwezesha Mamlaka za Majisafi na Majitaka katika miji kujitegemea katika kugharamia uendeshaji na uwekezaji katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kukamilisha miradi mikubwa ya ukarabati na upanuzi wa Majisafi na Majitaka Dar es Salaam, na ule wa kupeleka maji katika miji ya Kahama,

Shinyanga na vijiji vitakavyopitiwa na bomba kutoka Ziwa Victoria.

Afya

Mheshimiwa Spika:

Serikali ya Awamu ya Tatu imechukua hatua mbalimbali kuboresha sekta ya afya kwa lengo la kuinua kiwango cha ubora wa huduma za afya, kuzisogeza karibu zaidi na wananchi na kuongeza uwajibikaji wa watumishi wa sekta hii. Tutaendeleza hatua hizo. Huduma ya afya kwa kina mama na chanjo mbalimbali kwa watoto zitaendelea kutolewa na kuboreshwa zaidi. Tunataka kila mtoto wa Kitanzania apate chanjo zote zinazostahili.

Aidha, tutaimarisha mtandao wa kusambaza dawa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati, pamoja na kuendelea kuongeza bajeti ya ununuzi wa dawa na vifaa vya tiba. Ukarabati wa hospitali, vituo vya afya na zahanati utaendelea. Kadhalika tutaendelea kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali zaidi mijini na vijijini. Tutaziendeleza na kuziimarisha huduma za Mfuko wa Bima ya Afya na zile za Mifuko ya Afya ya jamii ambazo zimeonyesha mafanikio makubwa. Kwa kutambua kuwa kinga ni bora kuliko tiba tutakazania pia elimu ya afya.

Mapambano dhidi ya malaria na kifua kikuu yatapewa msukumo maalum.

UKIMWI

Mheshimiwa Spika:

Nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la UKIMWI. UKIMWI ni janga la kitaifa na dunia kwa ujumla. Janga hili limekuwa likiathiri utendaji na kupunguza nguvukazi ya Taifa. Hivi sasa wananchi karibu wote wanaelewa UKIMWI pamoja na athari zake, na njia za kuepuka kuambukizwa. Hata hivyo, wapo baadhi ambao wamesikia na kuelimishwa lakini bado wanasita kukubali kuwa hili ni janga kubwa. Tutaendeleza jitihada za kuhamasisha na kutoa elimu ya UKIMWI kwa wananchi wote ili kuhakikisha kuwa kila mwananchi anao uelewa sahihi wa janga hili Aidha, Serikali itatenga. rasilimali zaidi, na kushirikiana na wadau mbalimbali, kuongeza upatikanaji wa dawa za kurefusha maisha na kupunguza makali kwa watu wengi zaidi walioathirika na UKIMWI.

Makundi Maalum

Mheshimiwa Spika:

Katika jamii yetu yapo makundi maalum ambayo Serikali inao wajibu wa kuwasaidia. Kundi la kwanza ni la watoto yatima. Hivi sasa kutokana na

athari za UKIMWI, idadi ya yatima inaongezeka sana nchini. Katika baadhi ya maeneo, watoto hawa ndio wakuu wa kaya. Tunahitaji wadau mbalimbali wakae pamoja na kuandaa mipango endelevu ya kuwalea na kuwasaidia watoto hawa. Watoto yatima wanahitaji elimu, lishe bora, huduma za afya, makazi na upendo sawa na watoto wengine wa Kitanzania. Ni wajibu wa jamii kuwapa mahitaji hayo.

Serikali itachukua hatua za kuhakikisha kuwa watoto yatima wote nchini wanapata fursa za kupata elimu pamoja na huduma za afya. Nitataka wizara nitakayoiunda kusimamia masuala ya watoto iwasilishe Serikalini katika muda mfupi ujao mpango endelevu wa kushughulikia mahitaji ya kundi hili linaloongezeka katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika:

Kundi jingine maalum ni lile la walemavu. Zipo hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa kuwapa fursa walemavu kutumia vipaji vyao ili kujitegemea. Changamoto kubwa kwetu kama Taifa ni kuwa tuache kuwanyanyapaa na tuwaone kuwa ni binadamu wenzetu. Serikali itachukua hatua za kuhuisha sera na sheria ili kutoa upendeleo maalum kwa walemavu katika utoaji wa huduma mbalimbali

na vilevile katika kuweka mazingira yatakayowapa fursa ya kutekeleza majukumu yao kwa jamii.

Mheshimiwa Spika:

Lipo pia kundi la wazee wetu. Wazee ni hazina kubwa ya Taifa lolote. Wao ndio watiotujengea misingi ya Taifa tuliyo nayo hivi sasa. Zipo hatua zilizochukuliwa za kuwawezesha kupata huduma za afya bila malipo na kwa wale wa mijini kutotozwa kodi ya pango kwa zile nyumba wanamoishi wenyewe. Jamii yeyote iliyostaarabika inalo jukumu la kuwaenzi na kuwatunza wazee. Jukumu la kwanza ni la wanafamilia na wanajamii wa karibu wa mzee anayehusika. Wasikwepe jukumu hilo asilia, na la mila za Kiafrika. Serikali itahakikisha kuwa kunakuwepo utaratibu na mipango itakayowawezesha wazee kupata huduma muhimu kwa wepesi zaidi na kwa gharama nafuu, kwa kuzingatia taratibu, mila na utamaduni wa jamii zetu.

Mheshimiwa Spika:

Katika suala la jinsia, Serikali inatambua bayana na inaahidi kuzingatia nafasi ya wanawake katika maendeleo. Tutaongeza, awamu kwa awamu, ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na nafasi nyingine za maamuzi. Tutaendelea kuwahamasisha wanawake

wazitumie fursa za kisiasa katika nyanja mbalimbali, zikiwemo za uchaguzi katika ngazi zote, bila kusahau kuongeza nafasi na fursa katika ngazi za uteuzi kwenye utawala, uongozi na menejimenti ndani ya Serikali na Taasisi zake. Kadhalika, tutatekeleza ahadi ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Tutatengeneza na kutekeleza mikakati kabambe kwa ajili ya kuwasaidia wanawake wajikwamue na umaskini na uduni wa maisha.

Utalii

Mheshimiwa Spika:

Utalii ni moja ya sekta ambazo ni mhimili wa uchumi wa nchi yetu hivi sasa. Serikali yangu inakusudia kuendeleza sekta hii ili iongeze mchango wake kwenye pato na maendeleo ya taifa letu. Haitoshi kujigamba, peke yake, kuwa Tanzania ina mbuga kubwa na nzuri za wanyamapori, milima, mabonde na fukwe zenye mchanga mweupe. Ni kweli tunapaswa kuulinda na kuuendeleza urithi huu lakini zaidi ya hayo tunapaswa kuutumia urithi huu kwa manufaa ya nchi yetu. Tunapaswa kuboresha huduma kwa watalii kama vile malazi, chakula, usafiri na bidhaa za kumbukumbu za kuwauzia watalii. Tunapaswa kukaribisha wawekezaji wa ndani na nje watakaojenga hoteli zenye hadhi ya kimataifa kuanzia nyota nne hadi tano. Tunahitaji

kujenga miundombinu ya kuwafikisha watalii katika maeneo ya kitalii kwa urahisi. Tunapaswa kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya utalii ili tuongeze idadi ya watalii na mapato kutoka utalii.

Hifadhi ya Mazingira

Mheshimiwa Spika:

Serikali ya Awamu ya Nne itatoa msukumo maalum kwa hifadhi ya mazingira kwani athari zake pale tulipopuuzia zinaonekana wazi. Mvua haba, rasilimali maji inazidi kupungua, na ukame unaongezeka. Serikali itaendelea kuthamini na kulizingatia suala hili, pamoja na kutoa elimu kwa wananchi ili kuongeza uelewa wao kuhusu hifadhi ya mazingira. Tutaiongezea Wizara inayohusika na mazingira uwezo na mamlaka ya usimamizi. Tutaendeleza kampeni ya upandaji miti na kuhimiza tabia ya kutokata miti ovyo, au kuchoma misitu ovyo. Ili kupunguza mahitaji ya kuni na mkaa tutaendeleza matumizi ya nishati mbadala.

Miaka arobaini tu iliyopita, Tanzania Bara ilikuwa bado na misitu mingi, chemchem na vijito vingi. Sehemu kubwa ya ardhi yake ilikuwa imefunikwa na majani. Leo hali ni tofauti, na kwenye baadhi ya maeneo hali inatisha.

Mheshimiwa Spika:

Uchomaji misitu na ukataji ovyo wa miti vimesababisha vyanzo vya maji kukauka, mito kupungua maji na baadhi ya viumbe kuathirika na kutoweka. Hatuwezi kuendelea kuwa watazamaji au washangaaji wa vitendo hivi vya hujuma dhidi ya misitu na uhai wa taifa letu. Na wala uhuru wa Mtanzania kuishi popote katika nchi yake haujumuishi pia uhuru wa kuhairibu mazingira sehemu fulani na kuhamia sehemu nyingine. Hakuna uhuru wa kaharibu mazingira kwa namna yeyote ile. Serikali ya Awamu ya Nne maagiza yafuatayo:-

1. Kila kijiji kipande miti katika vyanzo vya maji;

2. Wizara ya Ujenzi ihakikishe miti inapandwa pembeni mwa barabara na katika maeneo karibu na madaraja;

3. Wizara yenye dhamana ya maliasili iweke utaratibu mzuri, unaofuatiliwa na unaopimika, wa upandaji miti na majani;

4. Wizara yenye dhamana ya ardhi ihakikishe machimbo ya mchanga na kokoto hayako katika maeneo karibu na vyanzo vya maji au katika mabonde na kingo za mito;

5. Wizara ya Madini ihakikishe inasimamia vizuri na kuyatolea taarifa za kila mwaka maeneo yote yenye machimbo ya madini ili kufuatilia na kujihakikishia kuwa wachimba madini wanazingatia matakwa ya leseni zao za uchimbaji madini na hasa masharti ya hifadhi ya mazingira;

6. Wananchi wanaoishi katika maeneo yenye viwango vizuri vya mvua za kutosha waongeze bidii na kasi ya kupanda miti;

7. Wizara yenye dhamana ya mazingira iandae ripoti za kila mwaka kuhusu hali ya mazingira nchini ikijumuisha mafanikio na changamoto;

8. Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji zitekeleze kwa vitendo agizo la siku nyingi la kupanda miti ya vivuli na matunda; na,

9. Watu binafsi, mmoja mmoja, au katika makundi, waanzishe kampeni ya kupanda miti kama zao la biashara.

Mheshimiwa Spika:

Yapo maeneo ambayo lazima zichukuliwe hatua maalum za kulinda na kuhifadhi mazingira

kwani hali imeanza kuwa mbaya sana hata kuanza kuhatarisha ustawi na maendeleo ya sekta nyingine. Eneo mojawapo ni Bonde la Mto Ruaha ambalo linahusisha vyanzo vya mito yote mikubwa nchini. Tumeshuhudia hali ya bwawa la Mtera inavyoendelea kuwa mbaya. Aidha, mto Ruaha Mkuu umeanza kukauka katika baadhi ya maeneo. Itabidi uongozi wa Serikali katika ngazi zote uwajibike zaidi kuhakikisha kuwa uharibifu wa mazingira unaosababisha hali hii ya kutisha unakomeshwa.

Eneo jingine ni lile linalozunguka Ziwa Victoria. Hivi sasa tunatekeleza mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Mkoa wa Shinyanga. Taarifa za kitaalamu zinaonyesha kuwa pamoja na umuhimu wa ziwa hilo, uchafuzi wake unaongezeka. Serikali itahakikisha kuwa uongozi wa mikoa yote inayozunguka ziwa hilo unashitikiana na taasisi za kitaifa na kimataifa na wananchi kuhifadhi ziwa hilo linalotegemewa na idadi kubwa ya wananchi wetu.

Uchumi Unaopaa

Mheshimiwa Spika:

Baada ya mafanikio ya Awamu ya Tatu, haitarajiwi kuwa Serikali ya Awamu ya Nne italegeza

kamba na kupuuza misingi iliyotuletea mafanikio tunayojivunia. Najua mengi yamesemwa na watu wanaodai wanamfahamu Jakaya Mrisho Kikwete na jinsi atakavyolegeza mambo. Napenda kuwahakikishieni kuwa watu hao wamepotea sana.

Wakati wa kampeni wapo baadhi ya wapinzani waliothubutu, kwa kukosa shukrani, kusema ati Serikali ya Awamu ya Tatu ilikuwa inatekeleza sera zinazobuniwa Washington. Serikali ya Awamu ya Nne haitaogopa kubuni na kutekeleza sera na mikakati ya maslahi kwa ukuaji wa uchumi na maisha bora kwa kila Mtanzania ati kwa vile zinaungwa mkono au kufadhiliwa na nchi tajiri na mashirika ya fedha ya kimataifa.

Hatutafanya lolote lisilo na maslahi kwa taifa letu kwa kuwaogopa au kutaka kujipendekeza kwa wakubwa hao. Lakini vile vile hatutaacha kufanya lolote la maslahi kwa taifa na Watanzania kwa vile tu linaenda sambamba na ushauri wa mashirika ya fedha ya kimataifa. Hatutafanya maamuzi kwa kutaka kupendwa; lakini tutafanya kila maamuzi kwa kigezo cha msingi cha maendeleo na maslahi ya taifa.

Mheshimiwa Spika:

Mbali ya kusukumwa na hoja ya kukuza uchumi haraka ili kupiga vita umaskini, tunasukumwa pia na ukweli wa nguvu za utandawazi na ushindani mkubwa katika masoko ya kanda na ya kimataifa. Hivyo basi, sote tuunganishe nguvu zetu ili tuongeze uzalishaji, tuongeze uwekezaji, tuongeze mauzo nje, tuongeze ubora wa mazao na huduma zetu na tuongeze kasi ya ukuaji wa uchumi wetu ili upae. Hakuna kurudi nyuma. Kasi mpya inayozungumziwa ni ya kusonga mbele na siyo kuserereka na kurudi nyuma kwa kasi.

Michezo, na Burudani na Utamaduni

Mheshimiwa Spika:

Michezo ni furaha. Michezo ni muhimu kwa afya zetu. Watanzania wanapenda sana michezo, ila furaha imekuwa inawakwepa kwa timu zetu kutokufanya vizuri. Lazima tutoke huko, na inawezekana. Tuwe makini kuendeleza michezo. Tutahimiza maendeleo ya michezo shuleni, na pale iniapowezekana katika sehemu za kazi. Shule ziwe mahali pa kubaini vipaji vya sanaa na michezo.

Tutaviwezesha vyama mbalimbali vya michezo ili Tanzania we mshiriki mkubwa, na si msindikizaji, katika mashindano mbalimbali ya michezo

ulimwenguni. Pamoja na hayo nitaanzisha mjadala wa kitaifa wa kuendeleza michezo nchini. Wadau wote washiriki, na Watanzania, tukubaliane juu ya mstakabali wa michezo nchini mwetu.

Tutaendeleza sekta ya utamaduni na burudani kwa ujumla. Miongoni mwa mambo ambayo tutayaangalia kwa karibu ni haki na maslahi ya wasanii ili kazi kubwa waifanyayo iwe na tija kwao.

Mheshimiwa Spika:

Lugha ya Kiswahili imeanza kupata umaarufu Afrika na duniani. Umoja wa Afrika umekubali Kiswahili kuwa moja ya lugha zake kuu. Aidha Nchi za Kanda ya Maziwa Makuu zimekubali kutumia na kutendeleza lugha ya Kiswahili. Serikali ya Awamu ya Nne itahakikisha kuwa juhudi hizi zinaendelezwa na kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inakua nje ya mipaka ya Afrika.

Mipango miji

Mheshimiwa Spika:

Kuendeleza miji ni jambo tutakalolipa uzito unaostahili ili tuwe na miji mizuri, safi na salama. Sote tumeona jinsi ambavyo dhana ya mipango miji inavyopuuzwa na kukiukwa na baadhi ya wananchi wetu, manispaa na halmashauri zetu. Mifano ya

ukiukwaji wa kanuni bora za mipango miji ni kama ifuatavyo:-

1. Nyumba na kuta zinajengwa katika maeneo ya mikondo ya maji;

2. Makazi ya watu yanaanzishwa katika maeneo ya hifadhi ya barabara;

3. Maeneo ya wazi, ya bustani na michezo kwa watoto wetu yanagawiwa kwa watu binafsi;

4. Mifugo inawekwa, na hata kuchungwa, mijini karibu na makazi ya watu;

5. Majumba marefu yanaruhusiwa kujengwa katika maeneo ambapo huduma za majitaka hazitoshelezi;

6. Majumba ya ghorofa yanajengwa katika maeneo ambapo pana makazi ya nyumba za kawaida na pasipotakiwa kuwa na ghorofa zaidi ya moja;

7. Makazi yanaanzishwa pasipo kuweka mifumo mizuri ya barabara na huduma nyingine muhimu hasa za maji taka na usafi wa mazingira;

8. Maeneo kwa ajili ya huduma za maduka, masoko, hospitali, shule, na maeneo ya ibada na makaburi, ama yanatengewa maeneo finyu au husahauliwa kutengwa, ama yakitengwa bado yanamegwa kwa ajili ya matumizi mengine; na,

9. Utupaji taka na mifuko ya plastiki hufanywa ovyo.

Mheshimiwa Spika:

Tusipozuia hali hiyo, na kuirekebisha, miji yetu itakuwa kama pori la majengo yasiyo na mpangilio wala huduma zinazohitajika. Serikali ya Awamu ya Nne itazitaka Halmashauri zote zishughulikie jambo hili haraka inavyowezekana.

Ujenzi na Utunzaji wa Bairabara

Mheshimiwa Spika:

Serikali za Awamu zilizotangulia zilisimamia ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikijumuisha barabara, vivuko na mad araja. Kwa kuzingatia hoja ya kuunganisha nchi na kuibua maeneo mapya yenye uwezo wa kiuchumi, Serikali ya Awamu ya Nne itaendeleza kwa kasi upembuzi yakinifu, usanifu, na ujenzi wa barabara na madaraja yote yaliyoorodheshwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005.

Nishati

Mheshimiwa Spika:

Nishati ni sawa na chembe za damu mwilini. Serikali ya Awamu ya Nne itatoa kipaumbele katika kuboresha na kuendeleza upatikanaji wa nishati ya uhakika na rahisi vijijini na mijini. Tutapanua wigo na aina ya vyanzo, vya umeme na nishati kwa jumla i1i kuwa na nishati ya kutosha na yenye gharama nafuu kukidhi mahitaji ya uzalishaji viwandani, utoaji wa huduma za kijamii, na matumizi ya nyumbani. Tutayashughulikia kwa kipaumbele cha juu matatizo ya sasa yahusuyo upatikanaji wa umeme nchini.

Mheshimiwa Spika:

Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa Oktoba 2005 inasema wazi kuwa Serikali ya Awamu ya Nne itaharakisha mradi wa kupata umeme kutoka makaa ya mawe ya Mchuchuma. Na hivyo ndivyo tutakavyofanya. Aidha, Serikali ya Awamu ya Nne itafufua mipango ya umeme wa Mto Rusumo na *Stigler's Gorge*. Tutaharakisha pia upatikanaji wa umeme kutoka gesi asilia ya Mnazi Bay.

Mheshimiwa Spika:

Lengo la Serikali ya Awamu ya Nne pia ni kuendeleza kazi ya kufikisha umeme katika miji mikuu ya wilaya isiyo na umeme hivi sasa, kuongeza

kasi ya kupeleka umeme viiijini kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini, na kuiunganisha Mikoa ya Kigoma na Ruvuma katika gridi ya Taifa.

Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

Mheshimiwa Spika,

Awamu. ya Kwanza ya uongozi wa nchi yetu iliweka misingi endelevu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Misingi hiyo ni ujirani mwema, ulinzi wa mipaka yetu, kuwasaidia wakimbizi na kuwa mtetezi wa wanyonge. Awamu zilizofuatia zimefanikiwa kuendeleza misingi hiyo. Serikali ya Awamu ya Nne nayo itaendeleza misingi hiyo pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje ambayo inalenga zaidi kwenye diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika:

Baada ya kuundwa kwa kamati ya kaharakisha Shirikisho la Jumuiya ya Afrika Mashariki tuna imani kwamba mapendakezo yake na malengo tuliyojiwekea yatafikiwa kwa muda uliopangwa. Serikali ya Awamu ya Nne itaendeleza kwa dhati mazungumzo haya ih kuhakikisha tunakuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki litakalotunufaisha sote sawia. Serikali ya Awamu ya Nne pia itaendeleza ushiriki wetu na uhusiano wetu na Jumuiya ya

Maendeleo ya Nchi zilizopo Kusini mwa Afrika (SADC) ili kutimiza malengo tuliyojiwekea. Serikali yangu itaelekeza nguvu zake katika kuhakikisha kuwa nchi yetu inajipanga vizuri kunufaika na fursa za Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC.

Mheshimiwa Spika:

Tanzania ni mwanachama na mwanzilishi wa Umoja wa Afrika. Serikali ya Awamu ya Nne itahakikisha kuwa Tanzania inaendelea kushiriki kwa ukamilifu na kuwa mwanachama mwaminifu wa Umoja wa Afrika. Tutachangamkia fursa ya kuendeleza mapambano ya kujikwamua na umaskini na kujiletea maendeleo kama ilivyoainishwa katika programu ya Mshikamano Mpya wa Maendeleo katika Afrika (NEPAD).

Mheshimiwa Spika:

Serikali ya Awamu ya Nne itahakikisha kuwa Tanzania inaendelea kushiriki kwa ukamilifu katika utatuzi wa migogoro Barani Afrika, na hususan katika mchakato wa amani na maendeleo kwenye Kanda ya Maziwa Makuu. Tunataka amani ya kudumu na utulivu ili kupunguza mzigo wa wakimbizi kwa nchi yetu, na kuongeza fursa za biashara na ushirikiano wa kikanda.

Mheshimiwa Spika:

Tanzania itaendelea kushiriki kwa ukamilifu kwenye shughuli za Umoja wa Mataifa. Hivi sasa nchi yetu ni mwanachama wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na kuanzia kesho kutwa, Januari 1, 2006, Tanzania itashika nafasi ya Urais wa Baraza hilo kwa kipindi cha mwezi mmoja. Katika kipindi hicho Tanzania inatarajia kuleta ajenda ya usalama na usuluhishi wa migogoro katika Eneo la Maziwa Makuu ili lijadiliwe na Baraza hilo. Lengo letu ni kutoa fursa kwa chombo hiki muhimu cha Umoja wa Mataifa kutafakari na kuchukua hatua madhubuti kukabili matatizo ya usalama na maendeleo ya eneo letu. Kadhalika, tutaongeza ushiriki wa Jeshi letu katika Majeshi ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika.

Ulinzi na Usalama

Mheshimiwa Spika:

Amani na utulivu wa nchi yetu ni moja ya agenda kubwa ya Serikali ya Awamu ya Nne. Maendeleo ya uchumi pia yanategemea sana utulivu wa nchi. Pamoja na matukio ya hapa na pale nchi yetu kwa jumla imetulia, na ni wajibu wetu kuuendeleza utulivu huu, Rwa kufanya yafuatayo:

1. Kujenga mazingira mazuri ya kazi kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama;

2. Kuendeleza juhudi za kuwa ina Majeshi ya Ulinzi na Usalama yaliyo imara yenye nidhamu ya hali ya juu na utii, na yenye utaalam na zana za kisasa;

3. Kuongeza uwezo wa vyombo vya ulinzi na usalama kupambana na ujambazi na kuzagaa kwa silaha ndogondogo ambazo zinatumika kufanyia uhalifu dhidi ya raia wema. Tatizo hili tutalivalia njuga.

4. Kuanzisha na kutoa vitambulisho vya uraia; na

5. Kuongeza kasi ya urejeshaji wa wakimbizi makwao.

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na juhudi hizi, kila Mtanzania mmoja mmoja, au katika makundi, analo jukumu la ulinzi wa nchi yetu. Tuwe tayari kutoa taarifa za watu tunaowahisi kuwa ni wahalifu ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao mapema iwezekanavyo.

Hitimisho

Mheshimiwa Spika,

Waheshimiwa Wabunge:

Napenda kuwashukuru tena wananchi wote kwa kunikubali na kunichagua niwe Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi niko tayari kuwatumikia Watanzania wote kwa moyo mkunjufu na kwa unyenyekevu mkubwa.

Nitaunda Serikali itakayodumisha umoja, amani na utulivu. Aidha, nitajitahidi kutoa uongozi wenye ufanisi na uadilifu mkubwa; Serikali itakayowaongoza na kuwawezesha Watanzania.

Mheshimiwa Spika:

Naishukuru tena Serikali ya Awamu ya Tatu kwa kuweka misingi imara na madhubuti ya kutuelekeza na kutuwezesha kujenga Tanzania inayojitegemea zaidi na yenye ustawi kwa wananchi wote. Lengo letu kuu ni kusukuma ukuaji wa uchumi kwa ARI MPYA, NGUVU MPYA na KASI MPYA ili kuwa na MAISHA BORA KWA KILA MTANZANIA.

Mheshimiwa Spika
Waheshimiwa Wabunge.

Nimesema mengi. Kwa leo inatosha. Ninamalizia kwa kuwahakikishieni kuwa nafahamu vizuri sasa ukubwa wa heshima na uzito wa majukumu niliyokabidhiwa na Watanzania wenzangu. Ninafahamu matarajio ya Chama changu, Chama Cha Mapinduzi. Nitaongoza kwa dhati utekelezaji wa ahadi zetu kwa wananchi, na kwa dunia. Ninayajua matarajio ya Watanzania wenzangu walipoitikia wito wa ari mpya,, nguvu mpya na kasi mpya. Ninayajua matarajio ya nchi jirani, bara la Afrika na dunia kwa Awamu ya Nne ya uongozi wa taifa letu. Ninajua wahisani wetu na wawekezaji, wa ndani na nje, wananisikiliza kwa makini, wakitaka kujiridhisha iwapo nitavijaza viatu alivyoniachia Rais wetu mpendwa wa Awamu ya Tatu, Benjamin William Mkapa. Nitajitahidi ingawa ni vikubwa kwangu.

Kwenu nyote, na kwao wote, naahidi kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, na kwa ushirikiano na Bunge hili na wananchi kwa ujumla, kuwa naweza kutimiza matarajio ya kila mmoja.

Tanzania yenye neema tele inawezekana. Maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana. Kila mmoja wetu atimize wajibu wake.

Mungu Ibariki Afrika.
Mungu Ibariki Tanzania.
Ahsanteni kwa kunisikiliza.